

WORD OF LIFE CHURCH AND MINISTRIES

UHUSIANO WA MWAJIRIWA NA MAELEZO YA UHUSIANO WA MAADILI

Twapenda kila mwajiriwa wa Word of Life na Home of Hope kufahamu vyema matarajio ya tabia yake.

SISI NI KANISA MOJA KATIKA MAENEO MENGI ULMIWENGUNI! Word of Life Church and Ministries ina makao makuu huko Red Deer, Alberta, Canada, Mchungaji Mel na Heather Mullen ndio waanzilishi na Wachungaji wakuu. Mchungaji Mel pia ni Rais wa Halmashauri ya wakurugenzi wa Word of Life Church and Ministries inayotoa mwongozo wa kisheria kwa matawi yote ya Word of Life ulimwenguni. Word of Life Church and Ministries haianzishi makanisa huru (yanayojisimamia), bali kama mti, tunaanzisha “matawi” (yani yaliyo sehemu ya ibada ya Word of Life) yaliyounganika kwa mti.

Mali yote, ikiwemo mashamba, majengo na vifaa ni mali ya Word of Life Church and Ministries – Red Deer, Alberta, haijalishi ilipatikana vipi.

Mchungaji Brian Thomson ni Mkurugenzi wa kimataifa juu ya matawi yote ya Word of Life katika Rwanda, Kenya, India, Congo, na ni Mkurugenzi Mwanzilishi wa huduma za Home of Hope ulimwenguni. Wachungaji waangalizi na viongozi wengine wamewekwa katika kila nchi kusaidia kutoa uongozi bora katika inchi hizo. Ingawa tamaduni ya nchi yeyote ni bora katika kuanzisha na kudhibitisha matawi ya Word of Life, lengo la Word of Life Church and Ministries ni kuzalisha DNA ya Word of Life katika maisha ya uongozi wa matawi na utendakazi wake. Maamuzi mengi hufikiwa kupitia hatua za kujadiliana na maombi, wakati mwingine ni maagizo kutoka kwa Mchungaji Mel Mullen au Mchungaji Brian au mtu yeyote aliyepewa mamlaka kutoa maagizo kwa niaba yao. Waajiriwa wote wanapaswa kufuata maagizo hayo.

MAADILI

Waajiriwa, viongozi na wachungaji walioko na watakaojiunga watarajiwa kuwa na nidhamu ya kibiblia ya kiwango cha juu katika mienendo yao na kudumisha uadilifu takatifu. Viongozi wote wapaswa kuwa watendaji kazi kwa bidii, kuwa vielelezo wa nguzu, kuepuka ulevi, kutoa zaka kamili kwa mapato yao yote kanisani jumapili na kuwa nguzo ya kanisa, wakitoa uongozi siyo kwa maneno tu bali kwa vitendo, kuepuka ufidia wa kifedha, na tabia legevu jinsi ilivyo orodheshwa katika Biblia vitabu vya Kutoka 20:1-17, Matendo ya Mitume 6, 1Timotheo 3, na Tito 1, Wagalatia 5:14-26.

Wakati wowote, mwajiriwa au kiongozi wa Word of Life Church and Ministries na Home of Hope hafuati mfano wa Biblia wa mashemanzi, wazee wa kanisa au mchungaji, au hawezi kuendelea kufanya kazi katika moyo wa umoja na mchungaji Mkuu wa Word of Life International au mchungaji mwangalizi wa matawi ya Word of Life aliyechaguliwa katika nchi hiyo, au na waajiriwa wengine, **anulizwa kuwacha kazi** na kudumisha amani kwa ajili ya kanisa la Mungu alilolifia Yesu.

Kila kiongozi na mwajiriwa wa Word of Life na Home of hope yapaswa awajibike kutumia vyema fedha na rasilimali aliyokabidhiwa na kutoa hesabu ya kila pesa na rasilimali anayosimamia.

Twaomba waajiriwa wote kukoma kuwaendea au kuulizia msaada wowote kutoka kwa wageni wa kimataifa wanaokuja kusaidia miradi, kwa njia ya kibinafsi au kutumia simu au mtandao, au kwa njia yoyote inayoonyesha ishara ya kutaka kusidiwa – mfano: kuuliza kuombewa ukiwa na nia ya kupata kusaidiwa. Iwapo mgeni wa kimataifa yeyote atapeana pesa kwa hiari yake au msaada wowotea, Mchungaji Brian apaswa kuarifiwa kwa njia ya barua pepe. Tunakuuliza pia umjulishe kiongozi msimamizi wako kipawa au msaada uliotolewa kwa ajili ya kanisa au mradi wa Home of Hope.

Kwamba nimesoma kwa uangalifu na kuelewa kanuni za maadili ye Word of Life na Home of Hope na mimi hapa nakubali kufuata maagizo yote na kujitolea kudumisha viwango vya nidhamu vinavyoandamana na imani, madhumuni na mambo ya dhamana ya Word of Life.

BAADA YA KUSOMA STAKABADHI HII KINGANAGA, TIA SAHIHI NA KUPEANA KWA KIONGOZI MWANGALIZI WAKO, AU KUPELEKA KWENYE KIKAO CHA VIONGOZI.

MAJINA YAKO _____

TAREHE _____

SAHIHI _____